# LBE Komputa Na Intaneti- Programme 9

Mwandishi: Richard Lough

Muhariri: Maja Dreyer

Tafsiri : Eric Ponda

**Wahusika:** Beatrice (Msichana wa Makamu), John ( Mvulana wa Makamu), Intaneti Sauti, Mtaalam ( Sauti ya Mwanamume kutoka studio.)

**Clips (English) to be overvoiced:** Daniel Gichuki ( Mtaalam wa Komputa mwenye umri wa makamu)

Sauti nyingine Sauti kutoka Studio.

**Package 9.1**

**Music – [Full up for 0:10 then fade under Intro]**

## Intro 9.1

Hujamba na karibu kwa kipindi kingine cha Learning By Ear, mfululizo wa vipindi vinavyotayarishwa na Deutsche Welle Radio kuhusu Komputa na Intaneti. Katika kipindi hiki cha tisa na cha mwisho katika mfululizo wa vipindi hivi, Beatrice na John wanajaribu kuchanganua uhalifu unaotokea katika matumizi ya mtandao wa Intaneti ulimwenguni. Kila siku matepali wa mtandao hujaribu kuiba anuani za watu na kuwatapeli watumiaji wa Tovuti mamilioni ya Madola. Je mtandao ni chombo kinachopendelewa zaidi na matapeli? Andamana nasi ujue ni kwanini na lengo lao kubwa lipi….

SFX_ Mtandao ukifunguliwa .

**1.Internet:** Habari John na Beatrice…

**2. John/Beatrice:** Hujambo Intaneti.

**3. Intaneti:** Je mumewahi kuwaona mwizi wa Benki wa kutumia silaha?

[SFX_King´ora cha Polisi]

**4. John:** Unamaanisha wezi wa silaha wanaoiba magunia ya pesa benki…?

**5. Beatrice:** Hapana.

**6. Intaneti :** Siajabu, hata mimi pia sikuamini kabla ya kuwasili kwa mtandao wa Intaneti.

**7. John:** Huh?

**8. Intaneti:** Kwa kuwa sasa muna anuani na mnaweza kutumia tovuti, kunatisho kubwa la uwezekano wa kulengwa na matapeli wa tovuti katika Mtandao.!

**9. Beatrice/John:** Eti nini ?!

**10. Intaneti:** Mnajua si rahisi kunichunga, kwa hiyo ni jukumu la watumiaji kurasa za tovuti kuhakisha usalama wao wao wenyewe katika mtandao.

**11. Beatrice:** Lakini ni vipi tunaweza kufanya hivyo?

**12. Intaneti :** Sawa, hayo tutayasikia katika sehemu ya pili ya kipindi hiki. Matapeli wa kurasa za tovuti wamewapora mamilioni ya madaola watumiaji wa mtandao na kusababisha hasara na uharibifu wa mabilioni..

**13. John:** Kwa hivyo, hawa matapeli hufanya vipi wizi huo?

**14. Intaneti:** Hutumia njia nyingi tu. Cha msingi wanachotaka ni pesa!. Na watafanya kila wawezalo kumshawishi mtumiaji wa tovuti au Mtandao wa Intaneti kutoa anuani yake na ***password***.

**17. John:** Lakini vipi? Mimi siwezi kutoa siri zangu.

**18. Intaneti** Wana njia nyingi tu, moja wapo ni kutumia tovuti ya uchunguzi maarufu kama ***Spyware.***.

**SFX_James_Bond_Anthem – if we can use it…**

**19. John:** Si ni uhalifu …

**20. Internet:** Ndio. Na matapeli hawa hutumia programu fulani ambayo huingia katika akaunti ya Mtu na kuiba maelezo yote kuhusu anuani na hata ***Password*** yake na kadhalika.

**21. Beatrice:** Hiyo ndio inayofahamika kama kashfa ya 419?

**22. Intaneti:** Ndio ! Kashfa ya 419 ni mfano mzuri wa wizi wa tovuti unaoendelea hasa Barani Africa. Wizi wa aina hii ulianzia nchini Nigeria kunako miaka ya 80. Tatizo langu kubwa ni, ongezeko la watu wanaotumia mtandao kwa kutuma barua pepe. Hatua hii ilipunguza gharama ya huduma hizi na hivyo matapeli wakapata fursa nzuri.

**23. John:** Nambari hizi za 419 zilitokana na nini?

**24. Intaneti:** Hizi zilitokana na kifungu cha sheria za kukabiliana na uhalifu wa kutumia udanganyifu nchini Nigeria..

**SFX_ Akiandika kwa Komputa**

**25. Intaneti:** Hebu tazama barua hii. Nimetoa kutoka jaa la barua taka kwenye komputa, katika moja wapo ya anuani za wateja! Soma….

**26. John:** ***( akisoma )*** “ Habari, Ninayo furaha kukujulisha kwamba nahitaji msaada wako kuhamisha Dolla milioni 47 kwa akaunti yako.”

**27. Beatrice:** *( Akisoma)* " Kiwango cha pesa hizi huenda ni kutokana na malipo zaidi ya kandarasi. Pesa hizo zimehifadhiwa katika Benki kuu ya Apex nchini Nigeria."

**28. John:** ***( Akisoma)*** " Iwapo unakubaliana na ombi hilo, tunachohitaji ni nambari ya akaunti yako, jina na anuani "

**29. Beatrice:** *[ Akicheka* ] Na watu huangukia mtego huu?

**30. Intaneti:** Bila shaka , ni jambo la kusikitisha sana.

**31. Beatrice:** Kwa hivyo tunapasa kufanya nini tunapopokea barua za aina hii?

**32. Internet:** Kwanza kabisa unapasa kufuta barua hiyo haraka iwezekanavyo **[SFX_Recycle_Bin]**. Pia kuna Tovuti hizi ambazo unaweza kuripoti visa vya ulanguzi wa aina hii.

**33. Beatrice** Je uhalifu wote wa kupitia mtandao unahusisha pesa?

**34. Intaneti:** Hapana, sio wote. Mara nyingine utakuta watu wananitumia, kutuma picha za watoto wakiwa uchi..

**35. John** Na pia na rafiki yangu ambaye aliwahi kuwasiliana na Mtu asiyemjua alipokuwa moja wapo ya vyumba vya mawasiliano ya moja kwa moja kupitia mtandao.

**36. Internet** Hilo ni tatizo jingine! Mtu anapasa kuwa muangalifu zaidi anapotumia mtandao. Unapokuwa na mawasiliano ya moja kwa moja kupitia Mtandao, mara nyingi humuelewi vyema mtu unayezungumza naye. Unaweza kudhania unazungumza na Mtu mzuri kumbe.. ..

**37. Beatrice:** Lakini katika siku za hivi punde kumekuwa na ongezeko la uhalifu wa kimapenzi.

**38. Intaneti:** Ndio, huwezi kujua. Kwa hivyo wakati unaponitumia, unapasa kuzingatia usalama wako wakati wote.

**39. John:** Huo ni ushauri mzuri!. Asante sana mtandao.

**Music – Full up for 0:10 then fade under ..**

**SFX_IAT_Gichuki_RoomTone**

**1. Beatrice** Nimefika katika majengo ya taasisi ya mafunzo teknolojia ya mawasiliano kuzungumza na Daniel Gachuki, mmoja wa wakufunzi katika chuo hiki kuhusu njia za kujikinga na matapeli wa mtandao wa Intaneti. Swali langu la kwanza kwa Daniel: Wakati tunapowasiliano kupitia mtandao, kunauwezekano wa kuacha baadhi ya maelezo yetu kwenye mtando huo bila ya sisi kujua?

**Clip: 9.2_Gichuki_1a**

Kwa kutumia mtandao wowote, kunauwezekano wa kurekodi baadhi ya habari ambazo umekuwa ukituma au kupokea..

**2. Beatrice:** Kweli, Vipi?

**Clip: 9.2_Gichuki_1b**

Kwa mfano tuna tovuti ambayo inafahamika sana miongoni mwa watumiaji wa huduma hizi uitwao ***Cookies.*** Wakati unapofungua ukurasa wa tovuti, na kuacha wazi ukurasa huo ukiwa na maelezo yako kama vile jina, anuani na Password, na labda tuseme umefungua ukurasa mwengine, ukurasa wa tovuti hii huhifadhi maelezo yako na ikiwa unatumia tovuti hiyo mara kwa mara, basi utakuta mara nyingine unafunguka bila kuandika maelezo yako katika ukurasa huo au kutumia anuani na ***Password*** yako. Kwa hivyo ukurasa wa tovuti hii ya ***Cookies***

hukuwezesha kufungua haraka ukurasa wako bila ya kurudia anuani ya tovuti unayotumia

**3. Beatrice:** Kwa kweli ukurasa huu ni wamaajabu?

**Clip: 9.2_Gichuki_3**

***Cookies*** ni ni ukurasa dhaifu.Kwanza ikiwa zitachwa kurasa hizi , basi mtu anaweza kuzitumia kupata habari zako na kuzitumia dhidi yako.

**SFX: Beep sound (should always be used to introduce the expert, like somebody answering in a quiz show)**

**4. Expert:** Habari Beatrice, mimi ni mtaalam, wako wa Studioni Je unafahamu kwamba wakati unapotumia Komputa yako Mtu mwengine anaweza kujua kile ulichokuwa ukifanya katika mtandao? Wanaweza kujua ni tovuti gain uliyokuwa ukitumia, na kanda za Video ulizokuwa ukitazama.. Pia wanaweza kupata maeleo kuhusu akaunti yako ambazo umekuwa ukitumia kila mara.

**5. Beatrice:** Ehh… sasa nimeanza kushikwa na wasi wasi. Lakini mara nyingine uanapasa kutoa maelezo yake kwa mtandao hata ikiwa hutaki mtu mwengine ajue. Daniel, Je kuna njia watumiaji wa tovuti wanaweza kukabiliana na tatizo hili?

**Clip: 9.2_Gichuki_4**

Juhudi zinafanywa kuweka siri iwezekanavyo matumizi ya mtandao, yaani habari zilizoko kwenye mtandao ziwe haziwezi kufikiwa au kufunguliwa kwa urahisi au kusoma na kueleka.

**6. Beatrice:** Na je kuna njia nyingine watumizi wa mtandao wanaweza kujikinga na hali hii? Kwa mfano kuna njia ya kuweza kujingika dhidi ya matapeli wa mtandao kwa kutumia Komputa yako?

**Clip: 9.2_Gichuki_4**

Kunazo njia Fulani , kwa mfano kutumia programu inayofahamika kama ***Firewalls***. Unaweza kuweka programu hii ya Firewall kwenye komputa yako, ingawa nyingi ya komputa zinazotengenezwa sasa tayari zina programu hizi za Firewall ili kuchuja habari zinazoingia na kutoka Mtandao.

**SFX: Beep sound**

**7. Mtaalam:** Beatrice, hebu nikusaidie kuelewa zaidi suala hili.

**8. Beatrice:** Sawa. Asante...

**9. Expert:** Programu hii ya ***firewall*** ndio kinga yako ya kwanza kwa habari zako. Programu ya ***Firewall*** huwa kizuizi cha kukabiliana na uvamizi wowote kwenye komputa yako. Na hiyo ndio sababu ya kuitwa ***Firewall.*** Kazi yake hasa ni kame ukuta wa kukabiliana na kuenea kwa moto kutoka eneo moja hadi jingine.

**11. Beatrice:** **Sawa…..**

**12. Expert** Hii inamaanisha kuwa habari zote zinazopitia ukuta huu ni lazima zichujwe kwanza. Na habari zile ambazo hazitatimiza viwango vinavyohitajika basi zinazuiwa..

**13. Beatrice:** Sawa… Kwa hiyo Daniel, ukiwa na kinga hii ya ***Firewall***, je tunauhakika kwamba habari zetu zitakuwa salama dhidi ya uvamizi?

**Clip: 9.2_Gichuki_6**

Hatuwezi kuwa na uhakika wa asilimia 100, kwasababu mambo yanabadilika kila siku. Unaweza kuweka kinga ya ukuta au ***Firewall*** thabiti na kuwa na uhakika kwamba uko salama, kisha kukazuke aina nyingine ya Programu za uchunguzi au Spyware zenye uwezo zaidi kushinda nguvu za ukuta wako.

**Fade out SFX_ IAT_ Gicuki_RoomTone**

**Outro**

Na mpaka ndipo tunapofika mwisho wa kipindi cha leo na cha mwisho kwenye msururu huu wa vipindi kuhusu Komputa na Intaneti. Kukukumbusha kipindi cha leo kimezungumzia jinsi Mtu anavyopa kuwa na tahadhari dhidi ya matapeli wa Mtandao. Pia kumbuka mtandao unaokuuliza kuweka maelezo yako ya siri ni mtandao wa kuaminika na unakinga ya Firewall. Kila mara unapotumia mtandao wa Intaneti kumbuka kuwa kunawajasusi wa mtandaoni. Iwapo unataka kukisikilisha tena kipindi hiki au vyote tisa au kusikiliza na marafiki, tembelea mtandao wetu wa Intaneti www.dw-world.de/lbe. Tunakushukuru kwa kuungana nasi hadi wakati mwengine kwa kipindi kingine cha ` Learning by Ear` kwaheri.

MWISHO